**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
Dodoma

**APRILI, 2019**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, kuanzia tarehe 12 hadi 18 na tarehe 29 hadi 31 Machi 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake tarehe 26 na 27 Machi, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ina Mafungu 8 ya bajeti kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
v) **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama,
vi) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
vii) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na
viii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 2.1 Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Manyara na Arusha. Aidha, kwa kibali chako, Kamati ilifanya ziara maalum kwa ajili ya kutembelea na kukagua Ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara, kwa tarehe zilizoainishwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara ambao umezingatia matumizi ya TEHAMA. Aidha, Kamati imeridhishwa na ukarabati wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya ambao pia umezingatia matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri pamoja na utunzaji wa Kumbukumbu za Mahakama hiyo. Hivyo, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuanza kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mahakama nchini, kwa kuwa mfumo huo, utarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukaguzi wa Miradi husika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo juu ya ujenzi wa Mahakama 35 nchini, inayoendelea kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mgawanyo ufuatao:-

a) Mahakama Kuu Tatu (3),

b) Mahakama za Hakimu Mkazi Sita (6),

c) Mahakama za Wilaya Kumi na Nne (14), na

d) Mahakama za Mwanzo Kumi na Mbili (12)

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki cha fedha za maendeleo zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ujenzi wa Mahakama hizi unaweza kukamilika ifikapo Mwezi Julai, 2019. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupunguza usumbufu kwa baadhi ya Wananchi kutembea Kilomita nyingi kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, ilipokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahakama ya Tanzania kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021 wa Maendeleo ya Miundombinu kuhusu Ukarabati na Ujenzi wa Mahakama mbalimbali katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mikoa na Kitaifa pamoja na Nyumba za Makazi ya Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama nchini. Mpango huu pamoja na mambo mengine unalenga kuiwezesha Mahakama nchini kupunguza kwa kiasi kikubwa au kuondokana kabisa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo ya muhimili huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Mpango huu wa miaka Mitano (5) utatekelezwa kwa wakati, utaiwezesha Mahakama kujenga Jengo la Makao Makuu na Mahakama ya Rufani Jijini Dodoma, Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa Kumi na Mbili (12), Majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi Kumi na Saba (17), Mahakama za Wilaya Mia Moja na Nne (104) na Mahakama za Mwanzo Mia Moja (100), Nyumba za Majaji Kumi na Moja (11) na Nyumba za Mahakimu na Watumishi wengine Kumi (10).

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Mpango huu kwa kuwa unalenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wananchi, na pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

## 3.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 26 na 27 Machi, 2019. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu

Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2018. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Tisini na Saba, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Mia Nane Sitini na Mbili (27,097,646,862/=).** Hadi kufikia Februari, 2019 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba na Tisa,Laki Sita na Kumi na Sita Elfu, Mia Tatu na Saba(6,709,616,307)** sawa na **asilimia 25** ya lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kushuka kwa makusanyo ya maduhuli kunatokana na kubadilika kwa Sera ya gharama za utoaji haki nchini ambayo imefuta gharama za ada mbalimbali ambazo

zilibainika kuwa kikwazo kwa Mwananchi wa kawaida katika kupata haki mbele ya Mahakama. Hatua hiyo imeirejesha Mahakama katika nafasi yake ya kuwa chombo cha utoaji haki badala ya kuwa chombo cha kukusanya mapato yatokanayo na utoaji haki ili haki iweze kutolewa kwa kila Mwananchi bila kujali uwezo wake kiuchumi na haki hiyo ipatikane kwa gharama nafuu na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na mabadiliko hayo na inaipongeza Mahakama kwa kurahisisha na kuweka mazingira rafiki ya utekelezaji wa Ibara ya 13(1) ikisomwa pamoja na Ibara ya 107A(2)(a) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu utoaji haki nchini kwa Wananchi wote bila ya kujali hali yao kiuchumi.**

### 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tano, Milioni Mia Saba Ishirini na Sita, Laki Saba Sitini na Tatu Elfu (145, 726,763,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Saba, Milioni Mia Moja Sabini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Tatu (77,173,293,000)** zilikuwa ni za Mishahara na **Shilingi Bilioni Sitini na Nane, Milioni Mia Tano Hamsini na Tatu, Laki Nne Sabini Elfu(68,553,470,000)** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari 2019 Wizara na Taasisi zake zilipokea **Jumla ya Shilingi Bilioni Themanini na Saba, Milioni Mia Tano Sitini na Tatu, Laki Mbili Kumi na Nne Elfu, Mia**

**Nne Arobaini na Tano (87,563,214,445) sawa na asilimia 46%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo kwa kuwa hadi kufika Mwezi Februari, 2019 jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Tisa, Laki Tisa Hamsini na Nane Elfu, Mia Tisa Themanini na Mbili (36,169,958,982)** sawa na **asilimia 51%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi mengineyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha zilizobaki zinapatikana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Fedha 2018/2019 na ihakikishe fedha zitakazoidhishwa na Bunge zinapatikana kwa wakati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.**

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini na Nne, Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu (44,767,219,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** ni fedha za

ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu (26, 767,219,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2019 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano (12,889,120,095/=) sawa na asilimia 29 %** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Saba (7,000,000,000/=)** sawa na **asilimia 38.9%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani. Aidha, fedha za Nje zilizopokelewa hadi Mwezi Februari, 2019 ni **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano (5,889,120,095/=)** sawa na **asilimia 22** ya fedha za nje zilizotengwa.

## 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Nje na Fedha hizo hazijatolewa kwa wakati na fedha zinazoonekana kuwa ni za uhakika zaidi ni fedha za ndani.

**Hivyo, maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali iendelee kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba**

**na Sheria hususan Miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.**

**Aidha, kwa kuwa Mahakama imedhihirisha utendaji bora na wakuridhisha katika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa kwa ufanisi mkubwa, Maoni ya Kamati ni kuwa, Miradi inayotekelezwa inaweza kukamilika kati ya Mwezi Mei hadi Julai, 2019 endapo kiasi kilichobaki cha Fedha za ndani kitatolewa kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.**

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeainisha maeneo

zaidi ya Hamsini (50) ya viapumbele kwa Taasisi zote zilizo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya kiwemo;

i) Kuendelea na Ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Wizara katika eneo la Mji wa Serikali, IHUMWA Jijini Dodoma,
ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sheria,
iii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa kutenganisha Mashtaka na Upelelezi,
iv) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi mbalimbali chini ya Wizara na Taasisi zake,
v) Kujenga na kuboresha Majengo ya Mahakama nchini,
vi) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria nchini,
vii) Kuwajengea uwezo Watumishi kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao, kuimarisha weledi na kuongeza tija kupitia mafunzo ya muda mfupi,
viii) Kuimarisha Mfumo wa uandishi na urekebishaji wa Sheria,
ix) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi,
x) Kuimarisha utoaji wa Elimu kwa Umma juu ya masuala ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora nchini,
xi) Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Wilaya na Mikoa nchini,
xii) Kuongeza udahili wa Wanafunzi katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ili kuongeza idadi ya Wataalam wa Sheria nchini,
xiii) Kuendelea na Mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahali pa kazi,

xiv) Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili itoe huduma kwa ufanisi,

xv) Kuimarisha Mifumo ya usimamizi wa mashauri na udhibiti wa ubora,

xvi) Kuimarisha uhusiano wa Masuala ya kisheria baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Kitaifa na Kimataifa,

xvii) Kuimarisha Mfumo wa Utatuzi wa mashauri ya kawaida na ya siku nyingi kwa lengo la kupunguza mlundikano,

xviii) Kuanza Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria,

xix) Kuimarisha upatikanaji haki kwa Watu wasio na uwezo na kuratibu utekelezaji wa wajibu wa nchi katika Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu, na

xx) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa kujenga na kukarabati Miundombinu ya Mahakama katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya Msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki,

uboreshaji wa Taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Milioni Thelathini na Tano, Laki Mbili Themanini na Nane Elfu (35,288,000/=).** Kiasi hicho ni sawa na asilimia 0.13% ya Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, kupungua kwa makadirio ya Maduhuli chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kunatokana na mabadiliko ya Sera ya utoaji haki nchini ambapo kwa sasa, gharama za ada mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na Mahakama zimefutwa ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa haki nchini kwa kila Mwanachi, kwa bei nafuu na kwa wakati.**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.1**

**JEDWALI NA.1: Mpango wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KUKUSANYWA 2019/2020 |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 1,002,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 14,432,000 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 16,520,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 |
| 59 | Tume ya Kurebisha Sheria | 0 |
| **JUMLA KUU** | | **35,288,000** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya tarehe 26 Machi, 2019***

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Tatu, Laki Tano Sitini na Tano Elfu,**

**(47, 283, 565,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Moja, Laki Tisa Themanini na Nne Elfu (25, 231,984,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Hamsini na Moja, Laki Tano Themanini Moja Elfu (22,051,581,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2.**

**Jedwali Na.2: Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,304,962,000 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 6,632,301,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 7,288,327,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 17,704,158,000 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 13,409,449,500 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 6,850,192,802 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 1,985,775,000 |
| **JUMLA KUU** | | **55,175,163,302** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Serikali ya Tarehe 26 Machi, 2019***

## 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zinaombewa **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Laki Tano Tisini na Nane Elfu, Mia Tatu na Mbili (7,891,598,302/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi Blioni 6.27 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 4.64% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.**

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko hilo limezingatia mahitaji ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutokana na vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hii ni pamoja na kuongeza bajeti ya Fungu 19; Ofisi mpya ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwemo bajeti ya Maendeleo kwa lengo la kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ndani na nje ya nchi kwa ufanisi zaidi ikiwemo kuimarisha Nguvu kazi ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na uwepo wa Ofisi hiyo sambamba na utendaji wake wa kazi kwa sasa, kwani ndani ya miaka miwili ya uwepo wa Ofisi hiyo, Serikali imeshinda kesi muhimu za madai ndani na nje ya nchi, na hivyo kurejesha**

**heshima ya nchi kwa viwango vinavyoridhisha na kwa uzalendo mkubwa.**

Aidha, Ongezeko hili la Bajeti ya Wizara hii pia imetokana na kuboresha Bajeti ya **Fungu 55;** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambapo Kamati imebaini ongezeko la **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Themanini na Nne, Laki Mbili Sitini na Sita Elfu, Mia Nane na Mbili (2,484, 266, 802/=),** ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 56.9%** ya Bajeti ya Tume hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa, Spika,** Kamati imebaini pia ongezeko la **Shilingi Bilioni 1.2** katika Bajeti ya Fungu 35; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ongezeko ambalo litaiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hususan katika ngazi ya Mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati imeridhishwa na maboresho katika Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa kuwa yamezingatia maoni na Ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.**

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

## 5.1 FUNGU 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

i) **Mheshimiwa Spika**, wakati wa ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilibainika kuwepo kwa changamoto ya Watumishi wa Mahakama wakiwemo Mahakimu kukaa kwenye cheo kimoja kwa muda mrefu bila kupandishwa daraja, na uwepo wa mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa upande wa Mahakimu ikiwemo ukosefu wa stahiki zenye kukidhi hali halisi ya maisha kwa Watumishi hao, Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatua changamoto hizo kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na stahiki nyingine kwa Watumishi wake wote ili kuchochea motisha ya utendaji kazi kwa Watumishi hao ikiwa ni pamoja na kuimarisha usalama wao wawapo kazini.

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kuwa, kwa sasa, Mahakama nyingi za Mwanzo zina Mahakimu wenye Elimu ya Shahada ya Kwanza ya Sheria na hivyo kuwa na uwezo wa kutosha kitaaluma kuendesha mashauri ya jinai na madai katika Mahakama za mwanzo nchini. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kuondoa ulazima wa Maamuzi ya Mahakama za Mwanzo kufanyika kwa kura za Wazee wa Mahakama na badala yake, Wazee wa Mahakama wawepo kushauri tu lakini ushauri wao usiwe wa lazima kiasi cha kuingilia maamuzi ya Hakimu yenye

kuzingatia Sheria za nchi, au Serikali ione umuhimu wa kuondoa Wazee hao au kwa namna itavyoona inafaa bila kuathiri maamuzi ya Mahakimu.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa ushauri wa Kamati ni kwamba, pamoja na uwepo wa mila na desturi katika jamii zetu zenye kuhitaji Wazee washauri katika baadhi ya mashauri kwenye ngazi ya Mahakama za Mwanzo, siyo mara zote ushauri wa Walio wengi katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo unaendana na matakwa ya Sheria, lakini pia, hatua hiyo itarahisisha utoaji haki kwa wakati katika Mahakama za Mwanzo ikiwemo kupunguza gharama za uendeshaji wa Mahakama hizo.

iii) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa wakati wa Ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Mahakama katika Mkoa wa Arusha, Wilayani Longido, Kamati ilibaini uwepo wa vitendo vingi vya uharifu katika Mpaka wa Tanzania na Kenya (Namanga), na kwa kuwa, eneo hilo halina Mahakama ya Mwanzo ambayo ingesaidia utoaji haki kwa haraka kutokana na makosa ya jinai yanayotokana na usafirishaji dawa za kulevya hususan mirungi na bangi baina ya nchi hizo mbili, Kamati inashauri, Wizara ya Fedha na Mipango iliridhie maombi ya Wilaya ya Longido kuhusu Jengo lililokuwa Ofisi za TRA litolewe kwa Mahakama ili Ofisi hizo zitumike kuwa Mahakama ya Mwanzo ya Namanga kwa lengo la kuharakisha utoaji haki mpakani hapo ili kuimarisha udhibiti wa vitendo vya uharifu na kulinda usalama katika Mpaka huo. Hatua hiyo inawezekana kwa kuwa, tayari TRA wamehamia katika Ofisi mpya katika *Kituo cha One Stop Centre* cha hapo hapo Namanga.

iv) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mahakama katika jitihada zake za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Kamati inashauri kuwa, Waheshimiwa Majaji kwa kushirikiana na vyombo husika, waendelee kutekeleza utaratibu wao waliojiwekea wa kutembelea Magereza pamoja na Mahabusu nchini ili

kujionea hali halisi ya Mlundikano wa Watuhumiwa na Wafungwa, kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa miongozo ya Mahakama kuhusu kusikiliza na kumaliza mashauri mbalimbali kwa wakati, kama sehemu ya utekelezaji wa moja ya vipaumbele vya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

v) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mahakama imeiridhisha Kamati na Umma wa Tanzania kwa ujumla kuhusu namna inavyoendelea kutekeleza Miradi 35 ya Ujenzi wa Mahakama katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini, ikiwemo matumizi mazuri na ya kuridhisha ya fedha inayotolewa na Hazina, na kwa kuwa, imebainika wazi kuwa endapo Serikali itatoa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi** kilichobaki katika bajeti ya Ujenzi wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Miradi hiyo inaweza kukamilika na kukabidhiwa kwa Mahakama ifikapo Julai, 2019. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu na ulazima wa kutoa kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili kuiwezesha Mahakama kukamilisha miradi husika kwa wakati kwa lengo la kuboresha mazingira stahiki ya utoaji haki nchini.

vi) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

## 5.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, pamoja na

kuboresha stahiki za Wansheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi wa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

## 5.3 Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji wenye tija kwa Ofisi hii ndani ya Miaka miwili ya kuanzishwa kwake, na kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na rasilimali ya kutosha, iendelezwe na kupewa stahiki zenye kuridhisha ili kuimarisha uwezo wa Mawakili wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslai ya nchi na kwa ufanisi zaidi.

## 5.4 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

i) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa, Ofisi hii kwa sasa inakabiliana na kesi nyeti za kijinai ambazo zinaweza kuwepo kwa mazingira hatarishi kwa Waendesha Mashtaka nchini, na kwa kuwa, nguvu kazi ya Ofisi hii inahitaji kuboreshewa stahiki zao mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi zaidi, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Ofisi hii ianze kutekeleza matakwa ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 ya Mwaka 2018 ambapo, Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430 pamoja na mambo mengine muhimu, inampa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka kuanzisha kitengo Maalum cha kukabiliana na maeneo Maalum yenye matukio sugu ya kiuahrifu ili kuhakikisha kuwa, maeneo hayo yanapewa kipaumbele katika usimamizi wa haki jinai kwa maslahi mapana ya nchi.

b) Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Huduma Maalum (Mfuko wa Dharura) chini ya Ofisi hii kwa mujibu wa

Sheria, ambao utapokea fedha moja kwa moja kutoka Serikalini na vyanzo vingine kama vilivyoainishwa na Sheria, ili kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi hii muhimu katika kuendesha mashauri ya haki jinai nchini hususan kusimamia na kuharakisha haki jinai katika maeneo yaliyobainika kuwa na matukio hatarishi nchini.

c) Serikali ione umuhimu wa kubakiza chini ya Ofisi hii **asilimia 10% ya fedha** zitakazokuwa zinaokolewa na Ofisi hii kutokana na kesi za ubadhilifu zitakazosimamiwa na Waendesha Mashtaka, ili fedha hizo ziingizwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa dharura wa Ofisi hiyo, kama ilivyo kwenye vyombo vingine nchini vyenye majukumu maalum kama ya Ofisi hii muhimu.

d) Ofisi hii ihakikishe kuwa, Majukwaa ya Haki Jinai ya Wilaya na Mikoa yaliyoanzishwa kwa Mujibu wa Sheria, yanatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwemo kutembelea na kukagua mlundikano wa Watuhumiwa katika Mahabusu zote nchini ili kubuni na kutekeleza Mpango Mkakati wa kuondokana na changamoto hiyo inayoathiri utoaji haki nchini na kuibua malalamiko kutoka kwa Wananchi. Hii ni pamoja na kuhakikisha dhamana zinazotolewa na Polisi zinatolewa kwa wakati kwa mujibu wa Sheria za nchi.

e) Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu katika kuratibu Mfumo mzima wa utoaji haki nchini baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi. Hatua hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na kuongeza uwigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine vya kiupelelezi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ofisi hii imetekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu, kuhusu kufungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji

haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na Wananchi, Kamati inashauri Serikali, kutoa fedha zote zilizoombwa na Ofisi hii kwa wakati, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuboresha Mishahara na stahiki nyingine za Waendesha Mashtaka wa Serikali nchini ili kutoa motisha kwa Watumishi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

## 5.5 FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kutekeleza kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati kuhusu kuboresha Bajeti ya Tume hii muhimu ambapo, kwa mwaka huu bajeti imeongezeka kwa zaidi asilimia 56% ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kwa kuwa bado yapo malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu, ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa Watu Magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha kwa wakati, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengewa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa Sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

## 5.6 FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Tume ya kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mfumo wa Sheria nchini unaozungumza lugha moja *(Uniformity of Law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima *(unnecessary Conflict of Law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji, kutokana na kazi kubwa ya kurekebisha Sheria mbalimbali iliyotekelezwa na Bunge kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2017 hadi Mwaka 2019.

## 5.7 FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria

i) **Mheshmiwa Spika,** Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi zote zilizo chini yake, kuhakikisha inaendelea kutekeleza Mpango wake wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki nchini pamoja na kusimamia mazingira wezeshi ya utoaji haki. Hatua hiyo, itarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu na hivyo kuchochea Maendeleo ya nchi. Hii ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kusimamia Misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora miongoni mwa Taasisi zote za kisheria zinazohusika na utoaji haki nchini kwa manufaa ya Wananchi wote bila kujali hali yao ya kijamii na kiuchumi.

ii) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa tayari Serikali na Vyombo vyake imeshahamia Dodoma, na kwa kuwa tayari Bunge lako Tukufu limeshatoa Baraka zake kwa kutunga Sheria ya kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Serikali yake, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kusimamia Mpango wa kujenga Jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania hapa Dodoma kama ilivyoainishwa katika Mpango kazi wa Miaka Mitano wa Mahakama ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa Mahakama zote nchini kulingana na Bajeti ya Serikali.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa Hekima na Weledi Mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mhe. Prof. Palamagamba J.A.M Kabudi, (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na tunamshukuru kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati wote alipokuwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, hivyo, tunamtakia utumishi uliotukuka kwa majukumu yake mapya.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mhe. Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, (Mb), kwa kupewa majukumu mapya ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na pia tuna mshukuru kwa ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Kamati, pamoja na timu yake ya Watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inawashukuru kwa ushirikiano wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika, Kamati hii itakuwa tayari muda wote kulisaidia Bunge lako Tukufu katika kusimamia Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha Taasisi hizo zinatekeleza Mipango yake ya Maendeleo kwa ufanisi mkubwa kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
13. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb- Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang’ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;

20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Dkt.Suzan Alphonce Kolimba, Mb – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kushukuru Watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
17 APRILI, 2019